# MOTO WA JEHANUM

**JOE CREWS**

# MOTO WA JEHANUM

---

# UKWELI ULIOPOTOSHWA WAFAFANULIWA

---

Na Joe Crews

(Hotuba Na. 15 ya Mambo Ya Kweli Yanayoshangaza)

Mfasiri:  M. Mwamalumbili

Hell-Fire, A Twisted Truth Untangled  - Kiswahili

# MOTO WA JENANUM

## UKWELI ULIOPOTOSHWA WAFAFANULIWA

Mojawapo ya masomo ya kitheolojia katika Biblia linalowafanya watu kuchanganyikiwa vibaya sana ni lile la Jehanum. Limepapaswa-papaswa tu na wachungaji na mapadiri na kupotoshwa maana yake na walei [waumini wa kawaida] mpaka neno hilo limegeuka na kujulikana sana kama tusi na kiapo cha kawaida. Kila mahali watu wanauliza maswali yale yale. Jehanum ni nini na iko wapi? Mwisho wa waovu ni upi? Je, Mungu mwenye upendo atawatesa watu vibaya sana milele hata milele? Je, mioto ile ya Jehanum itauchoma uovu uliomo ndani ya wenye dhambi milele hata milele?

Hayo ndiyo maswali yanaostahili kupewa majibu kamili ya Biblia, na yale mabishano yaliyopo juu ya somo hilo yasingepaswa kutukatisha tamaa katika kuifunua kweli yote kama ilivyo katika Kristo. Kwanza kabisa, tunahitaji kuelewa kwamba *iko mbingu ya kuipata na jehanum ya kuikwepa*. Yesu alifundisha kwamba kila mtu, ama ataokolewa, ama atapotea. Hakuna mahali pa katikati pa kusimama, wala hakuna tuzo [zawadi] zitakazotolewa mara ya pili. "Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika *tanuru ya moto*; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao." Mathayo 13:41-43.

Kwa kuzingatia hatima hizo mbili kwa watu wote waliopata kuzaliwa [hapa duniani], sisi tungekuwa na bidii nyingi jinsi gani katika kuitafuta njia ile ya kweli. Kristo alisema, "Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima." Usalama kamili peke yake kwa mtu ye yote ni kuchukua kwa usahihi kile alichofundisha Yesu juu ya Jehanum. Fundisho lake ndilo peke yake linaloweza kutegemewa kabisa na ndilo la kweli. Alisema kwamba wengine watatupwa motoni, na wengine watang'aa katika ufalme wake.

Ni jambo lisilo la kawaida kwa kiasi fulani, Kristo ameshtakiwa na viongozi wengi wa dini kwamba anafundisha uongo juu ya somo hilo. Wamemshtaki kwamba anafundisha kuwa roho isiyokufa inaruka na kwenda zake kutoka katika mwili wakati mtu anapokufa, ama inakwenda mbinguni, ama jehanum. Hayo siyo aliyofundisha Kristo hata kidogo. Kamwe hakutoa dokezo lo lote kwamba roho fulani isiyo na mwili hujitenga na mwili wakati mtu anapokufa. Na kwa hakika hakutoa wazo lo lote kuonyesha kwamba waovu hupata mateso makali milele na milele mara tu wanapokufa.

Hebu sasa na tupate mfano mmoja kuhusu kile Yesu alichofundisha hasa juu ya somo hili la jehanum. "Na mkono wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika ufalme u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako jehanum. Marko 9:43. Maneno hayo ya Bwana yanathibitisha bila kuacha kivuli cho chote cha mashaka kwamba *ni mwili unaokwenda motoni*, wala siyo roho fulani isiyoonekana. Katika Mathayo 5:30 alizungumza juu ya "*mwili … mzima*" usitupwe jehanum. Hii humaanisha mikono, miguu, macho, na sehemu zote nyingine za mwili huu unaoonekana.

Kinyume cha fundisho hilo la Kristo, mimbara za [wahubiri wa] siku hizi huvumisha habari zinazotoa picha za kusisimua za roho zinazofikirika tu ambazo huuacha mwili huu mtu anapokufa - yaani, roho zisizokuwa na mwili wala umbo lo lote. Mtazamo huo, japo unaweza kupendwa sana na watu wengi, ni kinyume na yale aliyofundisha Yesu. Zingatia vema, maana yule Bwana aliye

Mwalimu Mkuu alisema tena na tena katika vitabu vya Injili - ya kwamba *wale wanaotupwa katika moto wa jehanum watakwenda mle wakiwa na MIKONO, MIGUU, MACHO na viungo vyote vya mwili*. Hawatakwenda katika hali fulani ya nafsi iliyo nyepesi kama hewa ambayo haina umbo lo lote au kama roho.

Sasa tuko tayari kuyachunguza mambo makuu manne ya kweli toka katika Biblia ambayo huulizwa juu ya hatima ya [mwisho wa] waovu.

## ADHABU HUTOLEWA BAADA YA HUKUMU

Ukweli muhimu wa kwanza juu ya jehanum ni huu: WALE AMBAO HAWAJAOKOLEWA HAWAENDI MAHALI KO KOTE AMBAKO WANAPEWA ADHABU MARA TU WANAPOKUFA, BALI WANALINDWA KABURINI MPAKA SIKU YA HUKUMU WATAKAPOPEWA ADHABU YAO. Kristo aliufundisha waziwazi ukweli huo katika mfano unaojulikana sana wa ngano na magugu. Baada ya mwenye nyumba kupanda ngano katika shamba, mtumishi wake akaja na kutoa taarifa kwamba magugu yalikuwa yanaota miongoni mwa ngano. Swali lake likawa kwamba, je, ayang'oe magugu yale wakati yakiwa bado machanga sana. Jibu la mwenye nyumba lilikuwa ni hili, "La; msije mkakusanya magugu, na kuzing'oa ngano pamoja nayo. *Viacheni vyote vikue hata WAKATI WA MAVUNO*; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita *mkayachome*; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu." Mathayo 13:29,30.

Basi hebu na uyafuatilie maneno yake Kristo anapoeleza maana ya mfano huo: "Azipandaye zile mbegu njema ni Mwana wa Adamu [Kristo]; lile konde [shamba] ni ulimwengu; zile mbegu njema ni wana wa ufalme; na yale magugu ni wana wa yule mwovu; yule adui aliyeyapanda ni Ibilisi; *mavuno ni mwisho wa dunia*; na wale wavunao ni malaika. Basi, kama vile magugu yakusanywavyo na kuchomwa motoni; *ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia* [sio sasa mtu anapokufa]. Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika *tanuru ya moto*; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno." Mathayo 13:37-43.

Hakuna awezaye kuufanya mfano huo uwe rahisi zaidi kwa kuyapanua yale aliyosema Yesu. Uko wazi mno hata mtoto mdogo anaweza kuuelewa. Alisema kwamba yale magugu yaliwawakilisha waovu na ya kwamba *wangetupwa motoni "katika mwisho wa dunia*." Ilikuwa ni wakati wa mavuno ambapo kazi ile ya kutenganisha ingefanyika, na yeye alisema waziwazi kwamba "*mavuno ni mwisho wa dunia*." Yawezekanaje basi, kwa mtu ye yote kuyaelewa vibaya maneno hayo ya Kristo? Wazo zima la waovu kwenda motoni wanapokufa linapingana na mafundisho dhahiri ya Bwana wetu yasemayo kwamba *watatupwa motoni katika mwisho wa dunia*.

Kwa kuwa hukumu [adhabu] yao pia inatokea *baada ya Kristo kuja*, basi, tunaweza kuona jinsi ambavyo ingekuwa vigumu kabisa kwa mtu ye yote kuadhibiwa kabla ya wakati ule. *Haki inadai kwamba mtu aletwe hukumuni kabla ya kuadhibiwa kwake.* Petro anatangaza, anasema, "Basi, Bwana ajua kuwaokoa watauwa katika majaribu, na *kuwaweka wasio haki hata siku ya hukumu ili wapate kuadhibiwa*." 2 Petro 2:9, KJV. Je, hilo linaleta maana, au sivyo? Hebu tuseme mtu mmoja angeletwa mahakamani akishtakiwa kuiba, na hakimu aseme, "Mwekeni mbali kwa miaka kumi; baada ya hapo tutaendesha kesi yake." Hebu sikiliza, hata hakimu wa kibinadamu asingekuwa hana haki kiasi hicho! Angeshtakiwa kwa kitendo hicho. Hakika Mungu asingekuwa na hatia ya kufanya upuzi kama huo.

Tukiiruhusu Biblia itupe maana ya kile isemacho, basi, hapawezi kuwapo na shaka lo lote katika suala hili. Waovu "wanawekwa" mpaka lini? Mpaka "siku ya hukumu." Ili wafanywe nini? Ili wapate kuadhibiwa! Hii humaanisha kwamba *hawawezi kuadhibiwa kabla ya siku ile ya hukumu*. Je, hivi Biblia inatueleza sisi mahali wanapowekwa mpaka wakati ule? Kristo mwenyewe alisema, "Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo *watu WOTE waliomo makaburini* wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu." Yohana 5:28,29.

Jambo hilo ni dhahiri jinsi gani! Yesu alisema kwamba wema na wabaya *watatoka MAKABURINI MWAO kupokea, ama uzima, ama adhabu ya kutengwa na Mungu milele*. Hilo huonyesha kwamba kuanzia wakati ule wanapokufa hadi wanapotoka katika ufufuo hawapokei thawabu, wala adhabu yo yote. Yote hayo hutokea wakati ule wanapotoka mle. Wanawekwa mpaka siku ile kama vile Petro alivyodokeza, ila Kristo alionyesha waziwazi ni wapi watakapowekwa - "makaburini."

Endapo yanahitajika maneno yaliyo wazi zaidi ya hayo, basi, msikilize Yesu asemapo maneno haya katika Luka 14:14: "Utalipwa katika ufufuo wa wenye haki." Au msikilize tena asemavyo katika Mathayo 16:27, "Kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake; *ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake*." Ni lini itakapokuwa hiyo "ndipo"? Atakapokuja na malaika zake. Hakuna zawadi au thawabu inayotolewa kwa mtu mpaka katika ufufuo wa wenye haki, atakapokuja na malaika zake wote. Mafungu hayo yanauvunjilia mbali ubishi wote. Yakichukuliwa katika aya zake, hayana shaka lo lote juu ya maana yake, wala hayana maana iliyojificha.

Tena Kristo ananukuliwa akisema hivi katika sura ile ya mwisho kabisa ya Biblia, "Tazama, naja upesi, na *ujira wangu u pamoja nami*, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo." Ufunuo 22:12. Hapo anatukumbusha sisi kwamba "kila mtu" – yaani, kila mtu binafsi - atapokea ujira wa haki wakati ule Kristo atakaporudi duniani. Ayubu alitangaza "kwamba mwovu huwekwa hadi siku ya maangamizi. Watatoka katika siku ile ya ghadhabu." Ayubu 21:30, KJV. Danieli aliandika kwamba hao "*walalao katika mavumbi ya nchi wataamka* [watafufuka], wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele." Danieli 12:2.

Je! linaweza kuwapo shaka lo lote kuhusu mahali wanapowekwa waovu kabla ya kukabili ufufuo, hukumu, na adhabu yao? Sisi tunao ushuhuda wa Petro, Danieli, Ayubu, na Bwana mwenyewe. Hakuna nafasi ya kukwepa suala hili la msingi. Wanawekwa kaburini.

Sasa tunalifikiria jambo kuu la pili la kweli kuhusu jehanum: HAKUNA YE YOTE MIONGONI MWA WALE AMBAO HAWATAOKOLEWA ATAKAYETUPWA KATIKA MOTO WA JEHANUM MPAKA BAADA YA KUJA KWA YESU MARA YA PILI KATIKA MWISHO WA DUNIA. Japokuwa tumekwisha kuona tayari ushahidi thabiti juu ya pointi hii, hebu na tuangalie ushahidi zaidi. Akiwa anaeleza juu ya adhabu ya waovu, Yohana aliandika hivi: "Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile *ziwa liwakalo moto na kiberiti.* Hii ndiyo *mauti ya pili*." Ufunuo 21:8.

## HAKUNA MAUTI YA PILI KABLA YA UFUFUO

Hapo ndipo wale waliopotea wanaonekana katika mioto ya jehanum, wakipata adhabu yao kwa ajili ya dhambi zao. Na adhabu hiyo ni nini? "Mauti ya pili," asema Yohana. Je, unatambua jambo hilo kwamba linathibitisha nini juu ya waovu? Linathibitisha kwamba *hawatatupwa katika ziwa lile liwakalo moto na kiberiti* [jehanum] *mpaka baada ya ufufuo wao kutokea*. Watu hao wanakufa mauti ya pili katika moto huo, lakini *hawawezi kupatwa na mauti ya pili mpaka wapewe uhai wao mara ya*

*pili* [wafufuliwe]. Waliishi maisha yao ya kwanza katika dunia hii na kufa mauti ya kwanza, wakaingia kaburini mwao. Kabla hawajafa mauti ya pili ni lazima wafufuliwe - ni lazima wapewe uhai mara ya pili. Hilo, kusema kweli, ndilo hasa linalotokea mwisho wa dunia. Yesu alisema, "Watu wote waliomo makaburini watatoka." Basi, baada ya kupata uzima wao mara ya pili katika ufufuo , ndipo waovu hao watakapoadhibiwa kwa dhambi zao katika moto wa jehanum, "*hii ndiyo mauti ya pili*" [mshahara wa dhambi – Rum. 6:23]. Pamoja na hayo, mauti ya pili ni ya mwisho, yaani, *ni mauti ya milele* ambayo kutokana nayo *hapatakuwa na ufufuo* kwao. Lakini jambo la kulizingatia ni *wakati itakapotolewa hiyo adhabu ya moto wa jehanum* - ni baada ya ufufuo katika mwisho wa dunia. Haitokei wakati wa mauti ya kwanza [inayowapata wema na waovu – Ebr. 9:27] kama wengi mno walivyoshawishiwa kuamini.

Je, hivi Biblia inatueleza namna watakavyotupwa waovu katika lile ziwa la moto? Naam, inatueleza. Yohana anaeleza matukio ya kusisimua yanayotokea mwisho wa ile milenia [miaka elfu moja]. "Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake; naye atatoka na kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi, Gogu na Magogu, kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari. Wakapanda juu ya upana wa nchi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji huo uliopendwa [Yerusalemu Mpya]. MOTO [wa Jehanum] UKASHUKA KUTOKA MBINGUNI, UKAWALA." Ufunuo 20:7-9.

Hapo tunaona kwamba katika mwisho wa ile milenia waovu wote waliopata kuishi [katika dunia hii] watatoka katika ufufuo ule wa pili. Baada ya kueleza jinsi wenye haki watakavyokuwa hai na kutawala na Kristo katika kipindi kile cha miaka elfu moja, Yohana aliandika, akasema, "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu." Ufunuo 20:5. Wafu waliosalia, kusema kweli, walikuwa ni wale waovu, na ufufuo wao utampa Shetani nafasi ya kuendeleza vita yake dhidi ya Mungu na watakatifu wake. Anatoka kwenda kuyakusanya majeshi ya wale waliopotea ambao wamefufuliwa kutoka katika wafu. Anao watu wa kuwadanganya tena, naye anawahakikishia ya kwamba wanaweza kuushinda Yerusalemu Mpya ambao umeshuka chini kutoka mbinguni kwa Mungu (Ufunuo 21:2). Wanapotembea kijeshi na kuuzingira mji ule, waovu wale ghafula wanakatiliwa mbali [wanauawa] na moto ule ulao ambao unanyesha juu yao toka mbinguni. HUO NDIO MOTO WA JEHANUM AMBAO NDIO ADHABU YA MWISHO KWA DHAMBI.

## MAHALI ILIPO JEHANUM

Biblia inasema waziwazi kwa uthabiti kwamba moto huo unawala hao waovu papa hapa "juu ya upana wa nchi." Kila mwandishi wa Biblia anayezungumza juu ya somo hili la jehanum anaongeza maarifa mapya juu ya hiyo mauti ya pili ya wale waovu. Petro anaeleza hivi: "Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, *zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu*." 2 Petro 3:7. Kisha anaendelea kueleza habari ya ile siku ya Bwana itakayoviyeyusha viumbe vya asili kwa moto mkali sana.

Lugha ya Petro iko wazi sana kuhusu mahali pa adhabu kwa wale wasiomcha Mungu. Anasema kwamba *nchi hii* imewekwa akiba kwa moto ule utakaoleta hukumu na maangamizi kwa waovu. Adhabu yao itakuwa katika nchi [dunia] hii. Isaya alitangaza hivi, "Maana ni siku ya kisasi cha BWANA, mwaka wa malipo, ili kushindania Sayuni. Na vijito vyake vitageuzwa kuwa lami, na mavumbi yake yatageuzwa kuwa kiberiti, na ardhi yake itakuwa lami iwakayo." Isaya 34:8,9.

Nabii huyo anaonyesha picha ya sayari hii nzima ikifunikwa na moto ulao. Hata vijito na mavumbi vinageuzwa na kuwa lami inayolipuka na kuwaka moto mkali na kiberiti. Isaya anasema kwamba hicho ndicho kisasi chake Mungu na "thawabu" yake wakati wa mwisho wa pambano hilo.

Daudi anaongezea juu ya ushuhuda huo kwa maneno haya, "Awanyeshee wasio haki mitego, moto na kiberiti na upepo wa hari, na viwe [vitakuwa – KJV] fungu la kikombe chao." Zaburi 11:6. Zingatia kwamba anatumia karibu maneno yale yale kama Yohana na Petro katika kuelezea ajali itakayowapata waovu. Wote wanakubaliana kuhusu mahali pa adhabu hiyo (kuwa ni nchi [dunia] hii) na njia iliyochaguliwa kwa adhabu hiyo (moto).

Jambo hilo hutuleta kwenye ukweli mkuu wa tatu kuhusu somo hili la jehanum. JEHANUM KAMA MAHALI PA ADHABU ITAKUWA NI DUNIA HII AMBAYO ITAGEUZWA NA KUWA ZIWA LA MOTO KATIKA SIKU ILE YA HUKUMU. Lakini jambo hili pia huzusha maswali fulani ya kuvutia sana kuhusu ajali itakayowapata wale watakaopotea. Mojawapo ya maswali hayo yanayowachanganya sana watu na kuwaletea utata mwingi sana linahusu muda utakaotumika kwa adhabu hiyo. Je, ni kwa muda mrefu jinsi gani waovu wataendelea kuwa hai na kuteswa katika moto ule?

Hakuna awezaye kujibu swali hilo kwa usahihi kabisa kwa sababu Biblia inasema kwamba wataadhibiwa kulingana na kazi zao [matendo yao]. Hii humaanisha kwamba patakuwa na viwango vya adhabu. Wengine watateswa kwa muda mrefu kuliko wengine. Lakini jambo moja tuwezalo kusema kwa hakika kabisa ni hili - waovu hatawaendelea kuishi katika moto ule milele na milele.

## MOTO WA JEHANUM SI KWAMBA HAUNA MWISHO WAKE

Zipo sababu kadhaa zinazotufanya kuwa na hakika kabisa juu ya suala hilo. Kwanza kabisa, dunia hii pia inatangazwa kuwa itakuwa ndiyo makao ya mwisho ya wenye haki. Yesu alisema, "Heri wenye upole; maana hao *watairithi nchi*." Mathayo 5:5. Petro, baada ya kueleza habari za dunia hii ikilipuka kwa mshindo mkuu na kuteketea, aliona nchi mpya imejazwa na haki. "Lakini, kama ilivyo ahadi yake, *tunatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake*." 2 Petro 3:13.

Waovu hawawezi kuendelea kuishi katika sayari hii kwa sababu imeahidiwa, hasa ikiwa katika ukamilifu wake wote, kuwa itakuwa kwa ajili ya uzao wa kiroho wa Ibrahimu (Rum. 4:13). Baada ya kutakaswa kutokana na laana yake yote ya dhambi, itarudia tena katika hali ile ya milki [enzi] ya kwanza, na kulandana kabisa na mpango wa kwanza wa Mungu kwa nchi hiyo. Hatimaye itakuwa kama vile Mungu alivyokusudia iwe - yaani, itakuwa makao makamilifu kwa ajili ya watu wake walio wakamilifu.

Pili, waovu hawawezi kuendelea kuishi katika dunia hii kwa sababu hawajapata kamwe kumtegemea Kristo kwa uzima wao wa milele. Ni wale wenye haki tu wanaopokea karama ya uzima wa milele. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16. Lakini, je! ni vipi kwa wale wasiomwamini? Hakika wataangamia. Biblia inasema, "Mshahara wa dhambi ni mauti." Warumi 6:23. Tafadhali usikose kuielewa maana iliyoelezwa kwa urahisi katika mafungu hayo. Waovu kamwe hawaahidiwi kupewa uzima. Wanaahidiwa kupewa mauti - yaani, mauti ya milele. Ni wale wenye haki tu wanaoahidiwa kupewa uzima - yaani, uzima wa milele.

Lakini basi, kuna njia moja tu ya kuupata uzima usio na mwisho, na njia hiyo ni kwa imani katika Yesu. Yohana anaielezea kwa njia hii: "Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima." 1 Yohana 5:11,12. Hebu na nikuulize swali: Je! waovu wale katika ziwa lile la moto wanaye Mwana wa Mungu? Hasha. Basi, wangewezaje kuwa na uzima? Yohana anasema, "Nanyi mnajua ya kuwa kila mwuaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake." 1

Yohana 3:15. Je! wauaji wale walio katika ule moto wa jehanum wataendelea kuwa hai milele? Hasha.

Ungekuwa ni uzushi wa daraja la juu kabisa kuamini kwamba uzima wa milele ungeweza kupatikana toka katika chimbuko jingine lo lote zaidi ya Yesu. Je, waovu hao wangeupata wapi? Paulo anatangaza kwamba ni Yesu Kristo aliye"ufunua uzima na kutokuharibika, *kwa ile Injili*." 2 Timotheo 1:10. Maandiko yaliyovuviwa hayafunui chimbuko jingine lo lote la luzima wa milele isipokuwa kwa njia ya Injili ya Kristo. Fungu linapatikana wapi katika Biblia linaloeleza kwamba wanaweza kupewa uzima wa milele wale walio waovu? Waweza kusoma mara nyingi kuhusu wenye haki wakiupokea, lakini kamwe sio yule asiyeamini.

Paulo alisema, "Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala [hatutakufa] sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa." 1 Wakorintho 15:51-53.

Mafungu hayo yanasema habari za kikomo fulani katika wakati ambapo wenye haki watabadilishwa na kuwa viumbe wasiokufa. Wakati ule bado uko mbele. Unatokea Yesu arudipo, wakati wa parapanda ile ya mwisho, ufufuo utakapotokea. Hakuna mahali po pote katika Biblia tunaposoma kwamba waovu watabadilishwa kwa njia kama hiyo. Na hasa ni kwa sababu wao hawaipokei karama hiyo ya uzima wa milele, basi, hawawezi kuendelea kuishi katika ziwa lile la moto.

Ni wazo la kushangaza sana na lisilo na maana kuzua uongo kuhusu tukio hilo. Liko kinyume kabisa na Biblia, tena linachukiza sana mawazoni. Ezekieli alitangaza, alisema, "Roho ile itendayo dhambi itakufa." Ezekieli 18:4. Haidhuru sisi tueleweje juu ya hiyo roho ilivyo, hebu na tuikubali kweli hii ya Biblia iliyo rahisi kueleweka isemayo kwamba roho inaweza kufa kama matokeo ya dhambi.

Kama waovu wanaishi milele katika ule moto, basi, wanacho kitu kile kile walicho nacho wenye haki [yaani, uzima wa milele], isipokuwa wao wako mahali tofauti. Ni nani ambaye angeweza kuwapa huo uzima wa milele, kama siye Kristo peke yake? Yohana 3:16 analimaliza suala hilo kwa wazi na kirahisi mno. Wale wasiomwamini Mwana pekee WATAPOTEA [WATAANGAMIA]. Watakufa. Watapatikana na MAUTI YA PILI - yaani, mauti ya mwisho, mauti ya milele ambayo kutokana nayo hawataweza kufufuliwa kamwe. Ni adhabu isiyo na mwisho, adhabu ya milele, kwa sababu ni mauti isiyo na mwisho, yaani, mauti ya milele.

## MOTO USIOZIMIKA

Mmoja anaweza kuzusha swali hili: Ni vipi basi, kuhusu ule moto usiozimika ambao unawachoma waovu hao? Je, haimaanishi kwamba hautazimika kamwe? Kwa kweli, haimaanishi hivyo. *Kuzima* maana yake ni *kukizuia kitu kinachowaka kisiendelee kuwaka.* Hakuna atakayeweza kuizima mioto ile ya jehanum. Huo ndio moto wa ajabu wa Mungu. Hakuna hata mmoja atakayejiokoa kutoka katika moto huo kwa kuuzima. Isaya anasema hivi juu ya moto huo, "Tazama, watakuwa kama mabua makavu; moto UTAWATEKETEZA; hawatajiokoa na nguvu za mwali wa moto; hautakuwa kaa la kukota moto, wala moto wa kukaa karibu nao." Isaya 47:14. Baada ya kumaliza kazi yake, *moto huo utazimika.* Hakuna awezaye kujiokoa mwenyewe na mwali wake kwa kuuzima, ila hatimaye hakuna kaa la kukota litakalobakia. Hivyo ndivyo yasemavyo Maandiko.

Yeremia alitabiri kwamba Yerusalemu utateketezwa kwa moto ambao usingeweza kuzimwa (Yer. 17:27), lakini *uliteketezwa na kuwa majivu* (2 Nya. 36:19-21). Soma mafungu hayo na kuona jinsi Biblia inavyolitumia neno hili "kuzima." Halina maana ya moto usioweza kuzimika kamwe. Lina maana ile tu lisemayo, "usiozimika." Hauwezi kuzimwa na mtu ye yote.

Twaweza kusema nini, basi, juu ya maneno haya "milele" na "kuendelea pasipo kukoma" ambayo yanatumika kuelezea moto huo wa jehanum? Hakuna utata wo wote kabisa, au kinyume chake, wakati tunapoiacha Biblia yenyewe kutoa maelezo ya maneno yale yaliyotumika ndani yake. Neno hilo ni mfano wa kitu gani? Wengi hufanya kosa la kutumia maelezo ya siku hizi kuyafafanua maneno ya Biblia bila kuyahusisha na matumizi yake ya zamani ya aya zile zinazohusika (contextual usage). Jambo hilo hukiuka mojawapo ya kanuni za msingi za kufasiri Maandiko.

Ukweli ni kwamba moto wa milele hauna maana ya moto ambao hautazimika kamwe. Usemi uo huo umetumika katika Yuda 7 kuhusu maangamizi ya Sodoma na Gomora. "Kama vile Sodoma na Gomora, na miji iliyokuwa kando-kando, waliofuata uasherati kwa jinsi moja na hawa, wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, *imewekwa kuwa dalili*, wakiadhibiwa kwa "*moto wa milele*."

Ni dhahiri ya kwamba Sodoma bado haiendelei kuteketezwa leo. Bahari ile ya Chumvi (Dead Sea) inapafunika mahali pale iliposimama miji hiyo ya zamani. Lakini yenyewe iliteketezwa kwa "*moto wa milele*," nasi tunaambiwa kwamba ilikuwa ni mfano (dalili) wa kitu fulani. Je, ni mfano wa kitu gani? "Tena akaihukumu miji ya Sodoma na Gomora, akiipindua na *kuifanya majivu*, akaifanya iwe *ishara* kwa watu watakaokuwa hawamchi Mungu baada ya haya." 2 Petro 2:6.

Aha! maneno hayo! Yaani, kwamba ule moto wa milele ulioufanya Sodoma kuwa majivu ni mfano wa kile kitakachowapata waovu hatimaye. Kama fungu hilo linasema kweli, basi, moto ule ule ulioiteketeza Sodoma na Gomora utawateketeza pia waovu katika ziwa lile la moto. Huo utakuwa ndio moto wa milele. Je, hii ina maana kwamba utawafanya waovu kuwa majivu pia? Biblia inasema Ndiyo. "Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja ITAWATEKETEZA, asema BWANA wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi … Nanyi mtawakanyaga waovu; maana WATAKUWA MAJIVU CHINI YA NYAYO ZA MIGUU YENU; katika siku ile niifanyayo, asema BWANA wa majeshi." Malaki 4:1,3.

Hakuna maneno katika lugha yo yote yanayoweza kuyafanya maneno hayo kuwa na nguvu au kueleweka wazi zaidi. Moto huo wa milele unateketeza kila kitu milele zote. Hata SHETANI, ambaye ndiye Shina, hatimaye ATATEKETEZWA KABISA na kuwa majivu [Eze. 28:15-19; Isa. 14:10-20; Ufu. 12:7-12]. Ni ulinganifu ulioje huo ya kwamba tunapoiacha Biblia kueleza maneno yake yenyewe ndipo picha kamili inaonekana. Ni kuchezea maneno kijanja kulikoje huko ambako kungehitajika ili kuweza kuikwepa maana hiyo iliyo wazi ya maneno hayo. Lakini wale ambao katika maisha yao yote wamekuwa wakipendelea kuyafuata mapokeo [mafundisho ya wanadamu – Mk. 7:1-13; Mt. 15:1-14] wanaweza kuyasoma maneno hayo yasemayo, "itawateketeza … watakuwa majivu" na bado wao wakasisitiza kwamba waovu wangali hai na ya kwamba wanaendelea kuteseka motoni.

Hakika, yapo baadhi ya mafungu juu ya somo hili yaletayo utata, lakini tunagundua kwamba hayo yote yanapatana wakati yanapofikiriwa maneno yanayotangulia na yale yanayofuata (context) katika aya nzima, na wakati ule Biblia inapoachwa kujifafanua yenyewe.

Hata yale maneno ya Kristo katika Mathayo 25:46 hayaleti utata wo wote wakati ule tunapoichukua maana yake ile iliyo dhahiri. "Na hao watakwenda zao na kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele." Wengi wanasumbuliwa na usemi huo wa "adhabu ya milele," lakini basi, zingatia kwamba hausemi "kuendelea kuadhibiwa milele." Si kitu kama adhabu hiyo ni kitu gani, itadumu milele. Je, Biblia inatuambia sisi kwamba adhabu hiyo ni kitu gani? Ndiyo. "*Mshahara wa dhambi* ni *MAUTI*." Warumi 6:23. Kwa hiyo, Yesu alikuwa anasema tu kwamba *mauti hiyo ingedumu milele*. Isingeweza kufikia mwisho wake. Isingeweza kamwe kukatishwa kwa njia ya ufufuo.

Paulo anarahisisha zaidi kwa kusema maneno haya: "Katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; WATAKAOADHIBIWA

kwa …" Hebu sikiliza sasa, Paulo atatuambia sisi adhabu hiyo ni kitu gani. "WATAKAOADHIBIWA kwa MAANGAMIZI YA MILELE, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake." 2 Wathesalonike 1:8,9. Kwa hiyo, adhabu hiyo ni MAANGAMIZI [MAUTI] YA MILELE - yaani, maangamizi [mauti] yanayoendelea milele na milele. Kutokana na hayo [maangamizi/mauti] hapatakuwa na ufufuo, wala tumaini la uzima.

Lakini basi, ni vipi kuhusu yule funza asiyekufa? Wengi wameyasoma maneno hayo ya Yesu juu ya Jehanum, "ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki" (Marko 9:45,46). Wengine wameyafafanua na kusema kwamba funza huyo ni roho. Je, hivyo ndivyo Yesu alivyomaanisha? Hakuna po pote katika Biblia palipo na dokezo lo lote lisemalo kwamba roho ni kama funza.

Katika mfano huo Yesu alitumia neno "*Gehenna*" badala ya neno "Jehanum." Ilitukia kwamba Gehena palikuwa ni mahali halisi palipokuwa pakiwaka moto nje kidogo tu ya kuta za Yerusalemu. Bila shaka, wale waliokuwa wakimsikiliza Kristo waliweza kuuona moshi ukipanda juu kwa kujipindapinda toka katika lile Bonde la Gehena, ambako mizoga na takataka ziliendelea daima kuchomwa moto. Endapo kitu cho chote kiliangukia nje ya ndimi za moto zilizokuwa zinateketeza, basi, kililiwa mara moja na mabuu au funza. Picha dhahiri za matukio ya kuteketezwa kabisa kwa vitu vile zikiwa mbele ya macho yao, Yesu aliutumia ule moto wa Gehena kama kielelezo cha maangamizi kamili yatakayofanywa na moto ule wa Jehanum. Moto ule ulikuwa hauzimiki kamwe, na funza daima walifanya kazi yao juu ya mizoga ile - hiyo ni picha ya maangamizi kamili.

Labda fungu linaloeleweka vibaya kwa urahisi kuhusu jehanum ni dokezo la Yohana la moshi unaopanda juu "hata milele na milele" [Ufu. 14:11]. Kwa wale wasioyajua matumizi mengine ya kifungu hicho cha maneno katika Biblia ni kweli yanaweza kuwaletea utata mwingi sana. Lakini kulinganisha mafungu katika Agano la Kale na Agano Jipya huonyesha kwamba neno hili "*milele*" limetumika mara 57 katika Biblia kuhusiana na kitu fulani ambacho tayari kimeufikia mwisho wake. Kwa maneno mengine neno hili "milele" sio kila mara lina maana ya "pasipo mwisho."

Mifano mingi inayojulikana ingeweza kutajwa, lakini miwili au mitatu inafaa kuangaliwa. Katika Kutoka 21, masharti yamewekwa kuhusu sheria ya utumwa. Mazingira fulani yalihitaji kumtumikia bwana kwa maisha yote ya mtumwa yule. Katika hali kama zile sikio lake lilitobolewa kwa uma, na Maandiko yanasema hivi, "Ndipo atamtumikia *sikuzote* [*milele* – KJV]," fungu la 6. Lakini, je, ni kwa muda gani yule mtumwa angeweza kumtumikia bwana wake wa kibinadamu? Kusema kweli, kwa kadiri tu alivyoendelea kuwa hai. Kwa hiyo, neno hili "milele" [sikuzote] halikuwa na maana moja tu ya pasipo mwisho.

Hana alimchukua mwanawe Samweli na kwenda naye kwenye hekalu la Mungu, ambako [Samweli] ange"ka[a] huko *daima* [*milele* – KJV]." 1 Samweli 1:22. Lakini katika fungu la 28 tunaambiwa waziwazi kwamba "*wakati wote atakaokuwa hai* amepewa BWANA." Maana ya awali ya neno hili "milele" huonyesha kwamba ni *kipindi cha wakati kisichojulikana*. Kwa kawaida linaeleza kipindi cha wakati ambacho kitu fulani kinaweza kuendelea kuwapo chini ya mazingira yaliyopo. Hata kukaa kwake Yona katika tumbo la nyangumi kunaelezwa naye kama ni milele." (Yohana 2:6).

Mtu mmoja anaweza kupinga na kusema kwamba hili pia lingeweza kuwawekea kikomo cha maisha ya wenye haki kule mbinguni, kwa sababu wanaelezwa kama wanamtukuza Mungu milele. Neno ni lile lile linalotumika kwa waliookolewa na kwa waliopotea. Lakini tofauti kubwa sana ipo katika mazingira yao. Watakatifu wamepokea karama ya uzima wa milele. Maisha yao sasa ni sawa na yale ya Mungu. Uzima wa milele maana yake "kisichoweza kufa." Neno hili "milele" likitumika kuhusiana nao lingeweza kuwa na maana ile tu ya "pasipo mwisho," kwa sababu wao ni raia waliopewa tayari miili isiyokufa [1 Kor. 15:51-54]. Lakini neno hilo "milele" linapotumika kuwaelezea waovu, tunazungumzia habari ya viumbe wale walio na mwili unaokufa ambao wanaweza

kufa na ni lazima wafe. "Milele" yao inategemea jinsi miili yao inayokufa inavyoweza kustahimili katika moto ule unaowaadhibu kwa kadiri ya matendo yao.

## ROHO PAMOJA NA MWILI KUANGAMIZWA

Jambo hilo hutufikisha kwenye ukweli wa mwisho unaohusu ajali ya waovu. BAADA YA WALE AMBAO HAWATAOKOLEWA KUADHIBIWA KWA KADIRI YA DHAMBI ZAO, HUKU WAKIWA NA MIILI PAMOJA NA ROHO ZAO, WATAFUTILIWA MBALI HATA WASIWEZE KUWAKO KABISA MILELE HATA MILELE. Yesu alieleza jambo hilo kwa urahisi sana, "Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye KUANGAMIZA MWILI NA ROHO PIA KATIKA JEHANUM." Mathayo 10:28.

Katika nuru ya usemi huo, mtu anawezaje kuendelea kudai kwamba wafu wana miili isiyokufa? Yesu, awezaye kutoa karama ya uzima peke yake, anakana kwamba hakuna uwezekano wo wote kwa wale walio katika jehanum kuendelea kuishi humo katika umbile liwalo lote lile. Uhai wao utatoweka milele zote, na mwili wao utaharibiwa kabisa katika ndimi zile za moto.

Mtunga Zaburi aliandika maneno haya: "Bali wasio haki watapotea [wataangamia], nao wamchukiao BWANA watakuwa kama mafuta ya wana-kondoo: WATATEKETEZWA KABISA; KAMA MOSHI WATATOWEKA." Zaburi 37:20, KJV. "Maana bado kitambo kidogo ASIYE HAKI HATAKUWAPO, utapaangalia mahali pake wala HATAKUWAPO." Fungu la 10.

Maneno hayo ya ufafanuzi yenye nguvu sana katika lugha ya kibinadamu yametumika kuelezea maangamizi katika jehanum, lakini watu hao bado wanasisitiza kwamba waandishi hao hawana maana ile ile hasa kama vile maneno yao yanavyosema. "Angamiza", "teketeza", "choma kabisa", "kula", "mauti" - je! maneno hayo yana maana fulani iliyojificha, yaani, maana iliyo kinyume cha maneno hayo katika Biblia kuliko vile ilivyo katika vitabu vingine? Sisi hatuna sababu yo yote ya kufikiri hivyo. Ukweli ni kwamba theolojia imemfanya Mungu wetu mkuu mwenye upendo kuwa kama zimwi. Picha yake wanayoionyesha ni ya ukatili kuliko ule wa Hitler. Ingawa Hitler aliwatesa sana watu na kufanya majaribio juu ya miili yao, hatimaye aliwaachilia ili wapate kufa. Lakini ati Mungu ataziweka hai roho hizo zisizoweza kufa kwa kusudi la kuziona zikigaagaa na kupiga yowe milele hata milele, hivyo ndivyo wanatheolojia wanavyodai.

## HAKI YA MUNGU YATHIBITISHWA

Picha kama hiyo sio tu kwamba inauwakilisha vibaya sana upendo wa Mungu, pia inapotosha ukweli wa haki yake. Hebu fikiria kwa dakika moja hivi athari za fundisho hilo ambalo lingeipeleka mara moja na kuifungia katika jehanum isiyo na mwisho kila roho iliyopotea dakika ile ile aliyokufa yule mwovu. Tuseme kwamba mtu mmoja alikufa yapata miaka 5000 iliyopita akiwa na dhambi moja tu aliyoipenda sana katika maisha yake. Roho yake ingekwenda mara moja motoni na kuteswa vibaya sana milele hata milele. Kisha piga picha ya kifo kingine; kile cha Adolph Hitler, aliyesimamia mauaji ya mamilioni ya watu. Kulingana na fundisho hilo linalopendwa sana na watu wengi, roho yake pia ingeingia mara moja jehanum kuteswa humo milele na milele. Lakini mtu yule aliyepotea kwa sababu ya dhambi yake moja tu, ataendelea kuungua humo kwa zaidi ya miaka 5000 kuliko Hitler. Je, jambo hilo lingekuwaje la haki? Je, Mungu angeweza kutenda kwa njia kama hiyo? Jambo hilo lingeupinga usemi wa Biblia usemao kwamba kila mmoja ni lazima aadhibiwe kwa kadiri ya matendo yake [Luka 12:45-48; Ufu. 22:12].

Kuna mitazamo miwili inayovuka mpaka ambayo hivi sasa inaenezwa kote kuhusu adhabu ya waovu. Mtazamo mmoja ni ule *unaoamini kwamba ulimwengu wote utaongolewa* (Universalism),

ambao unadai kwamba Mungu ni Mwema mno kuweza kumwacha mtu ye yote kupotea. Mtazamo mwingine ni huo wa fundisho hilo linaloogofya mno la *mateso yasiyo na mwisho* ambayo yataendelea milele hata milele katika shimo refu lenye giza la utungu na mateso. Mitazamo hiyo yote miwili imepotoka. Ukweli uko katikati yake. Mungu atawaadhibu waovu kwa kadiri ya matendo yao, ila hataruhusu uovu wao uendelee milele kwa tendo lake hilo.

Mimi nasadiki kweli kweli ya kwamba watu wengi wanyofu wa moyo wamegeuziwa kando mbali na Mungu kwa sababu ya kuchukia kwao kutokana na njia hiyo ya kuielezea vibaya tabia yake. Hawawezi kumpenda mtu yule ambaye kwa udhalimu wake atawaweka waovu katika mateso yasiyo na mwisho bila kuwa na kusudi lo lote la maana mbele yake. Hakuna uwezekano wa kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida. Ni roho ile tu ya kutaka kulipa kisasi ambayo ingetumika kwa mpangilio kama huo usioelezeka. Je, Mungu yuko hivyo? Baada ya kuisikia kweli ya Biblia kuhusu jehanum, mwenyekiti mmoja wa benki alinikumbatia mabegani na kusema, "Joe, mimi nimekuwa muumini tena. Kwa miaka mingi nimekuwa nikisadiki kwamba sisi hatuna habari zinazomhusu Mungu, wala hatuwezi kuzijua, kwa sababu nilikuwa nimefundishwa kwamba Mungu angewatesa vibaya sana waovu milele na milele."

## HAKUNA MAUMIVU TENA WALA MAUTI

Siku moja hivi karibuni Mungu atautakasa ulimwengu mzima. Athari zote za dhambi zitatoweka milele. Hapatakuwa na dhambi, wala wenye dhambi, wala mwovu wa kutujaribu. Itakuwa sawa kabisa na vile alivyopanga Mungu hapo mwanzo.

Yohana alizielezea habari za makao yetu ya baadaye kwa maneno haya, "Naye (Mungu) atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." Ufunuo 21:4.

Je, hivi wewe unaweza kuona mwanya wo wote katika maneno hayo ya thamani ya kuwapo kwa mateso yo yote kwa upande wa mtu ye yote katika dunia yote iliyoumbwa upya? Mungu alisema kwamba kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena. Je, unaliamini Neno lake au unachagua kuamini mambo ya mwanadamu ya kukisia-kisia tu? Mafungu manne tu kabla ya kuiandika ahadi hiyo, Yohana alieleza namna waovu watakavyotupwa katika ziwa lile la moto. "Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto. Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita." Ufunuo 20:15; 21:1.

Ziwa la moto liko papa hapa juu ya uso wa sayari hii ya dunia yetu kwa mujibu wa Ufunuo 20:9. Lakini tafadhali zingatia kwamba mahali hapa wanapoteketezwa waovu *patapita*, na Mungu ataiumba upya nchi mpya mahali pake. Ndipo Ufunuo 21:2,3 unapoielezea Yerusalemu Mpya ikishuka, na fungu lile la nne linasema kwamba huzuni haitakuwapo tena, wala maumivu, wala kilio, wala mauti.

Ili maumivu zaidi yasipate kuwapo, haiwezekani pia kuwapo jehanum inayoendelea kuwaka milele. Mambo hayo mawili hayawezi kuchanganywa pamoja. Tungemshukuru Mungu kila siku ya kwamba mpango wake hatimaye utakomesha mateso yote. Shetani hatakuwapo hapa kusababisha maumivu hayo, naye Mungu anaahidi kwamba ufalme wake mpya hautakuwa na kivuli cho chote cha maumivu.

## JEHANUM HAIKUWEKWA KWA AJILI YETU

Jambo la mwisho, sisi tungeshangilia sana kwa sababu jehanum kamwe haikuwekwa kwa ajili yako wewe, wala kwa ajili yangu mimi. Yesu alisema kwamba "aliwekewa tayari Ibilisi na malaika zake" (Mathayo 25:41). Kama sisi tutajikwaa na kuangukia katika moto ule, litakuwa ni kosa letu kubwa

mno tuliloweza kulifanya. Ungeweza kwenda kule kwa kuukanyaga mwili wa Yesu Kristo uliopondeka kwa ajili yako [Ebr. 10:26-31], tena ungeweza kwenda huko, bila kujali upendo wa Baba, maombezi ya Roho Mtakatifu, na mvuto wa mbinguni wa mamilioni ya malaika. Swali lisilojibika kabisa ulimwenguni kote ni hili: "Sisi je! tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii?" Hakuna jibu kwa sababu sisi hatuwezi kupona isipokuwa kwa njia yake Kristo na msalaba wake.

Hakuna mtu ye yote atakayepotea ati kwa kuwa tu alitenda dhambi, kwa sababu kila mmoja ametenda dhambi. Hakuna atakayeachwa kwenda mbinguni ati kwa sababu alisema uongo, aliiba, au alizini. Sababu peke yake itakayomfanya mtu ye yote apotee ni ile ya kukataa kuipa kisogo [kuachana na] dhambi yake na kujitupa mikononi mwa Mwokozi mwenye upendo ambaye anasimama akiwa tayari kutusamehe na kutusafisha na udhalimu wote [Mithali 28:13]. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili KILA MTU AMWAMINIYE ASIPOTEE [ASIANGAMIE], BALI AWE NA UZIMA WA MILELE." Yohana 3:16.

---

**ANGALIA:** Maneno na mafungu yaliyo katika mabano haya [ ] yameongezwa kwa ajili ya ufafanuzi na kujifunza zaidi. Yasinukuliwe.